



KENYA PRIMARY SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT

DECEMBER ASSIGNMENT 2026

GREDI YA 6 – KISWAHILI LUGHA

STEPPING TO JUNIOR SCHOOL



Muda: Saa 2

MAELEZO YA MWANAFUNZI

Jina: _____ Shule: _____

Nambari ya Tathmini/UPI: _____ Tarehe: _____

MAAGIZO KWA MWANAFUNZI

1. Andika jina lako, nambari ya Tathmini/UPI na tarehe katika nafasi ulizopewa.
2. Hakikisha kuwa karatasi hii ina kurasa zote na hakuna swali lililokosekana.
3. Soma kila swali kwa makini kabla ya kuchagua jibu.
4. Jibu **maswali yote**.
5. Chagua jibu lililo sahihi zaidi kati ya A, B, C na D.

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.

Mbweha na Fisi ni viongozi wa mataifa yao. Fisi amekuwa akikabiliwa na mzozo wa uongozi katika taifa lake. Kwa hiyo, aliamua kumtembelea kiongozi mwenzake, Bwana Mbweha, ili kupata ushauri.

Mbweha: Karibu, Mheshimiwa Rais mwenzangu.

Fisi: Asante sana, ndugu yangu.

Mbweha: Masalkheri, ndugu. Habari za kwako?

Fisi: Bado hali ni mbaya. Mambo hayajatulia. Ndiyo maana nimekuja kwako ili unishauri.

Mbweha: Ni wazi kuwa vurugu hazitakoma hadi utekeleze tuliyoshauriana kwa simu. Kumbuka kuwa vijana wa kizazi hiki hawatikisiki.

Fisi: Vijana hawa wanaojiita Gen Z wanataka niondoke mamlakani. Hilo siwezi kulikubali kamwe. Wananilaumu kuwa nimeongeza ushuru na ninaendesha taifa kana kwamba ni kampuni yangu binafsi.

Mbweha: Hebu nieleze, msimamo wa jeshi lako ukoje?

Fisi: Idadi kubwa ya wanajeshi wananiunga mkono. Nimezungumza na wakuu wa vikosi mbalimbali na hawataki niondoke madarakani.

Mbweha: Wewe ndiye Amiri Jeshi Mkuu. Waite tena na uwaeleze kuwa jukumu lao ni kulinda nchi. Pia, tafuta njia za kikatiba za kutuliza hali na ushirikishe viongozi wa upinzani katika mazungumzo.

Fisi: (Kwa wasiwasi) Vijana hawa wa Gen Z si watu wa kubeza. Waliapa kuingia bungeni na wakafanikiwa. Naona huenda ikawa rahisi kuniondoa mamlakani.

Mbweha: Unakumbuka wakati wa kampeni uliwaahidi wananchi mambo mengi. Wamekuwa wakisubiri utekeleze ahadi zako na sasa wamechoka. Unapaswa pia kupunguza ufujaji wa mali ya umma.

Fisi: Wanyama wengi husema eti mimi ni mwongo. Siwaelewi. Wengine hata wanasema mavazi ya baadhi ya mawaziri wangu yanagharimu mamilioni.

Mbweha: Unapaswa pia kupunguza safari zako za nje ya nchi zinazotumia fedha nyingi za umma.

Fisi: Asante kwa ushauri wako. Sasa naondoka. Usiku mwema na asante kwa muda wako.

1. Mbweha alipomsalimia Fisi kwa kusema **“Masalkheri”**, Fisi alipaswa kujibu kwa kusema:

- A. Aheri B. Sijambo
C. Marahaba D. Jioni njema

2. Ni tatizo gani kuu linalojitokeza katika mazungumzo haya?

- A. Ahadi za Fisi kutotekelezwa
B. Fisi kukabiliwa na madai ya kuondoka uongozini
C. Safari za viongozi kwenda nje ya nchi
D. Vijana kukosa nafasi za ajira

3. Ni neno lipi katika mazungumzo haya **HALITUMIKI** kuonyesha cheo, heshima au hadhi ya mtu?

- A. Rais B. Ndugu
C. Amiri D. Wakuu

4. Ni kauli ipi ni ya kweli kulingana na mazungumzo?

- A. Jeshi lote lilikuwa limekataa kumuunga mkono Fisi.
B. Fisi alikuwa akiendesha serikali kwa kufuata matakwa ya wananchi wote.
C. Vijana wa Gen Z walikuwa tayari wamekubali kuingia serikalini.
D. Fisi alikiri kuwepo kwa matatizo kama ufujaji wa mali ya umma na matumizi makubwa.

5. Neno **“niondoke”** katika mazungumzo lina maana gani?

- A. Niondolewe kwa nguvu
B. Niache uongozi kwa hiari
C. Nibaki madarakani milele
D. Nikatae kuongoza

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

HAKUNA UBAGUZI

Sikieni niwambie, nyote mlo hadharani,
Hakuna tena kale, ya kujigamba mitaani,
Waume kuwekwa mbele, wake kuwa miguuni,
Kimpenda wa kiume, mpende naye wa kike.

Wote hao ni sawia, wakiwa ulimwenguni,
Aliwaumba Muumba, akawatoa kuzimuni,
Wacheni taasubi, za banati kuwalani,
Kimpenda wa kiume, mpende naye wa kike.

Jingine ni kufahamu, elimu iwe kichwani,
Na ujuzi wa kudumu, watu wakiutamani,
Daima takuwa tamu, wote watakuthamini,
Kimpenda wa kiume, mpende naye wa kike.

Tena ni uadilifu, tabia iliyo njema,
Kingia kati ya safu, uwe jinsia gani,
Halaiki takusifu, kwa mwenendo wa thamani,
Kimpenda wa kiume, mpende naye wa kike.

6. Kwa kuzingatia idadi ya mishororo
katika kila ubeti, shairi hili ni la aina
gani?

- A. Tarbia
- B. Tathilitha
- C. Tathnia
- D. Takhmisa

7. Kulingana na shairi, ni jambo gani
linaloweza kumfanya mtu athaminiwe
na watu?

- A. Elimu
- B. Ujuzi
- C. Tabia njema na uadilifu
- D. Jinsia yake

8. Ni upi **uta wa mshororo wa pili** katika
ubeti wa pili?

- A. Aliwaumba Muumba
- B. Wakiwa ulimwenguni
- C. Wacheni taasubi
- D. Akawatoa kuzimuni

9. Ni ujumbe gani mkuu unaopatikana
katika shairi hili?

- A. Watu wanapaswa kuepuka majigambo.
- B. Elimu ndiyo jambo muhimu zaidi maishani.
- C. Wanawake na wanaume wanapaswa kutendewa kwa usawa.
- D. Uadilifu pekee ndio unaomfanya mtu aheshimiwe.

Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yanayofuata.

Matatizo yalianza kumwandama Kisura alipoamua kujiunga na chuo cha mafunzo ya polisi huko Kiganjo. Alikuwa ameamua kuwa askari. Uamuzi wake haukuwapendeza watu wengi, hasa kwa sababu alikuwa msichana. Wengine walimhurumia wakihofia kuwa kazi hiyo ingeweka maisha yake hatarini.

Hata hivyo, Kisura alikuwa na malengo makubwa. Alitamani kuwa mpelelezi ili kusaidia kukabiliana na tatizo la ugaidi lililokuwa likiathiri nchi yake. Ingawa baadhi ya watu walimdharau, hakukata tamaa. Alijifunza mbinu mbalimbali za kukabiliana na magaidi.

Kweli, mtaka cha mvunguni sharti ainame. Bidii yake kazini haikupita bila kutambuliwa. Baada ya miaka michache, aliteuliwa kuongoza kikosi cha ujasusi nchini humo.

Kisura alianza kukutana na wananchi na kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kushirikiana na vyombo vya usalama katika kupambana na ugaidi. Pia alitembelea vijiji mbalimbali na kuwahamasisha wazazi kuruhusu watoto wao kujiunga na kikosi cha polisi.

Baada ya muda, wananchi walianza kubadilisha mitazamo yao. Wazazi wengi waliruhusu watoto wao kujiunga na polisi. Kisura alipata mafanikio makubwa kwa sababu ya ushirikiano kati yake, kikosi chake na wananchi. Hatimaye, juhudi hizo zilisaidia kukabiliana na ugaidi.

10. Ni changamoto gani kubwa ambayo Kisura alikumbana nayo mwanzoni?

- A. Kukataliwa na kikosi cha polisi
- B. Kudharauliwa kwa sababu ya uamuzi wake
- C. Kushindwa mafunzo ya kijeshi
- D. Kukosa ajira baada ya kuhitimu

11. Ni kauli ipi **SI YA KWELI** kulingana na kifungu?

- A. Kisura alikuwa mwanamke wa kwanza na pekee kujiunga na mafunzo ya polisi.
- B. Kisura alikuwa mfano mzuri katika jamii.
- C. Ushirikiano kati ya Kisura na wananchi ulisaidia kupambana na ugaidi.
- D. Kisura alikuwa kiongozi shupavu katika kikosi chake.

12. Neno **“kuwahamasisha”** katika kifungu lina maana gani?

- A. Kuwalazimisha watu kufanya jambo
- B. Kuwachochea watu kuchukua hatua fulani
- C. Kuwafanya watu waogope jambo
- D. Kuwadanganya watu kuhusu jambo fulani

Soma kisa hiki kisha ujibu maswali.

Fisi alikuwa akizunguka msituni akitafuta chakula. Usiku uliotangulia alikuwa amelala njaa. Ghafla, alimwona Kunguru akitua juu ya mti akiwa amebeba kipande kikubwa cha nyama.

Fisi alimeza mate. Alitamani kupata nyama hiyo ili atulize tumbo lake lililokuwa likinguruma kwa njaa.

“Masalkheri, rafiki yangu,” Fisi alimwamkia kwa upole. Kunguru hakujibu kwa sababu alijua kuwa akifungua mdomo, kipande cha nyama kingeanguka.

“Tazama! Naona nyoka mkubwa juu ya kichwa chako!” Fisi akasema akijaribu kumhadaa Kunguru.

Kunguru alitazama juu lakini hakuona nyoka. Alitambua kuwa Fisi alikuwa akijaribu kumdanganya na hivyo akazidi kushikilia nyama yake.

Fisi hakukata tamaa. Akafikiria hila nyingine.

“Mheshimiwa Kunguru, nimesikia kuwa wewe ni mwimbaji hodari sana. Tafadhali niimbie wimbo mmoja ili nisikie sauti yako nzuri,” Fisi akasema.

Kunguru alifurahi sana kwa kusifiwa. Akafungua mdomo wake na kuanza kuimba. Mara tu alipofungua mdomo, kile kipande cha nyama kikaanguka. Fisi akakinyakua haraka na kukimbia nacho.

13. Fisi alikuwa akitafuta nini msituni?

- | | |
|----------------------|-------------|
| A. Kipande cha nyama | B. Kunguru |
| C. Chakula | D. Mwimbaji |

14. Kisa hiki kinadhihirisha sifa gani ya Fisi?

- A. Ulafi B. Tamaa C. Uzembe D. Ujanja

15. Neno **“hila”** lina maana inayokaribiana na ipi?

- A. Mbinu ya kumdanganya mtu
- B. Ushindi mkubwa
- C. Msaada wa dharura
- D. Jambo la kawaida

SEHEMU B: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

16. Baada ya _____ mrefu, hatimaye mvua ilinyesha na wakulima wakaanza kulima mashamba yao.

- A. muda
- B. mudhaa
- C. mdaa
- D. mudha

17. Chagua neno linalofaa kukamilisha sentensi hii:

Baada ya mawingu kutanda, mvua _____ kunyesha.

- A. ilianza
- B. kulianza
- C. yalianza
- D. iliandaa

18. Wakulima walitumia jembe na trekta _____ mashamba yao kabla ya kupanda.

- A. kuandama
- B. kutayarisha
- C. kuyaandaa
- D. kuandaliwa

19. Ni alama gani ya uakifishaji inafaa kutumika baada ya neno **“walinunua”** katika sentensi ifuatayo?

Wazazi wangu walinunua vifaa vifuatavyo _____ mbegu, mbolea na dawa za kuua wadudu.

- A. :
- B. ;
- C. ,
- D. !

20. Kazi inayohitaji kutumia nguvu nyingi huitwaje?

- A. Kazi za kijungujiko
- B. Kazi za sulubu
- C. Kazi za ujumu
- D. Kazi za shokoa

21. Chagua neno linalofaa kujaza nafasi:

Chumba _____ anaishi Amina kina uchafu mwingi.

- A. ambayo
- B. ambacho
- C. ambao
- D. ambako

22. Chagua sentensi iliyo katika **wakati tegemezi**.

- A. Mama asipopika, hatutakula.
- B. Wanafunzi wamekuwa wakicheza uwanjani.
- C. Mkutano ungefanywa Alhamisi iliyopita.
- D. Shamba limelimwa na wakulima.

23. Katika sentensi hii, maneno **“huyu”** na **“yule”** ni ya aina gani?

Mchezaji huyu ndiye aliyefunga bao lakini yule aliumia.

- A. Vivumishi
- B. Vitenzi
- C. Viwakilishi
- D. Vielezi

24. Chagua kivumishi cha sifa katika sentensi ifuatayo:

Mtoto mtiifu humfurahisha mwalimu wake kwa mwenendo wake mzuri.

- A. wake
- B. mtiifu
- C. humfurahisha
- D. mwalimu

25. Maneno **mazingira, mafuta** na **marashi** yako katika ngeli gani?

- A. YA–YA
- B. I–I
- C. U–YA
- D. U–U

26. Chagua neno ambalo ni **nomino ya dhahania**.

- A. Maji
- B. Wema
- C. Kabati
- D. Meza

27. Sentensi “**Angalikujia angalinipata**” ina maana gani?

- A. Alikujia lakini hakunipata.
- B. Alikujia na akanipata.
- C. Hakujia lakini alinipata.
- D. Hakujia wala hakunipata.

28. Methali “**Nyangicha ni kobe safarini**” ina maana gani?

- A. Nyangicha hutembea kwa kasi.
- B. Nyangicha ni mvumilivu.
- C. Nyangicha hutembea polepole.
- D. Nyangicha ni mwepesi wa kufikiri.

29. Ni sentensi ipi iliyo na **kihisishi cha furaha**?

- A. Ewaa! Talia ameteuliwa kuwa waziri.
- B. Mama wee! Chakula chote kimemwagika.
- C. Ebo! Sitaki kumwona kijana huyo.
- D. Lahaula! Aliumia tena?

30. Chagua neno ambalo ni **tofauti** na mengine.

- A. Mwadhini
- B. Kaka
- C. Mwinjilisti
- D. Mtawa

MAJIBU

Na .	Jib u	Na .	Jib u
1	A	16	A
2	B	17	A
3	B	18	C
4	D	19	A
5	B	20	B
6	A	21	D
7	C	22	A
8	D	23	C
9	C	24	B
10	B	25	A
11	A	26	B
12	B	27	D
13	C	28	C
14	D	29	A
15	A	30	B